

Tutengenezeni Jiko la Enzaro

Ili kuhifadhi kawi na wakati



Tafsiri la Kwanza

Machi 1999

KENYA/JAPAN

Social Forestry Extension Model Development Project

JIKO LA ENZARO NI NINI?




Jiko la Enzaro ni aina ya jiko lililoendelezwa au kustawishwa na limetengenezwa kwa matofari na matope. Jiko hili lina shimo moja la kuwekea kuni na mashimo matatu ya kuwekea nyungu ambayo yana kimo cha urefu wa 50cm.

Jiko la Enzaro lina faida zifuatazo:-

1. Unaweza kuhifadhi utumishi wa kawi na utumishi wa kuni unaweza kupunguka kwa kiasi cha fungu la tatu au nusu cha jiko la mawe matatu. Hii ni kwa sababu unaweza kupikia kwa kutumia nyungu mbili au tatu kwa shimo moja la kuni lenye joto kali na tena lenye kuzuia kupotea kwa joto.
2. Unaweza kuhifadhi wakati wa upishi. Hii ni kwa sababu huna haja ya kushinda ukisukuma kuni kila wakati.
3. Unaweza kuhifadhi wakati wa kutafuta kuni. Hii jiko halihitaji kuni nyingi kama jiko la mawe matatu kwa hivyo hutafuti kuni mara nyingi.
4. Unaweza kujitengenezea jiko hili wewe mwenyewe kwa kutumia vitu vya kawaida kama vile matofali na matope ambavyo ni rahisi kutengeneza.
5. Ni rahisi kubadilisha kipimo na umbo la hili jiko. Unaweza kuamua kipimo chake kulingana na kiasi cha mahali pa kupikia. Unaweza kuchagua kuwa na mashimo mawili au tatu ya nyungu kulingana na mahitaji yako.
6. Ni salama kwa watoto wachanga. Hii ni kwa sababu hawawezi kufikia mahali penye moto.
7. Uko huru kutokana na hali ya kuumwa na mgongo. Huna haja ya kuinama sababu unaweza kupika ukiwa umesimama.
8. Joto linalokusumbua wakati wa kupika linapunguka. Jiko hili linatoa joto kiasi kidogo kuliko jiko la mawe matatu.
9. Linatoa moshi kwa mazao yaliyowekwa chini ya paa. Moshi na joto kiasi zinazofuka kwenye paa zatosha kuhifadhi matoleo ya mazao.

Uzuri wa jiko la Enzaro

Uzuri wa jiko la Enzaro



Ni rahisi kutengeneza jiko la Enzaro?

Ndiyo. Unaweza kujitengenezea mwenyewe
kwa muda wa nusuku.

Ebu tuanze!!

Vifaa na zana

Vifaa vya kazi


Jembe



Mtungi




Gari dogo lenye gurumdumu moja
(kimii)



Sepeto



Panga



ya kukata matofari

Mwiko




ama kipande kidogo cha
mabati ya kulainisha.


Zana

Kiasi cha vitu vya kutengeneza jiko kunategemea kipimo na umbo la jiko unalohitaji. Hiki kitabu kidogo kinaonyesha vitu unavyohitaji na jinsi ya kutengeneza jiko la Enzaro linalojulikana sana lenye mashimo matatu ya nyungu, kimo cha 50cm, urefu wa 110cm na upana wa 50cm.

Matofari




Mchanga



Maji




Mavi ya ng'ombe
ama mchanga mzuri



Jinsi ya kutengeneza Jiko la Enzaro

1. Matayarisho ya ardhi

- ① Chagua mahali pa kutengeneza jiko la Enzaro kulingana na mwelekeo wa upepo na pia hiari yako.



Jambo la kukumbuka

Mahali pa kutengeneza jiko la Enzaro patategemea kama utatengeneza la mashimo matatu au Mbili kulingana na mahitaji ya nyumba yako. Kwanza fikiriakiasi unachohitaji halafu anza kutayarisha sehemu ile.

- ② Kulima




- ④ Kusindilia



- ③ Kunyunyizia maji





- ⑤ Kukandika




2. Kutengeneza misingi

⑥ Kupanga matofari

⑨ Kufanya ⑥ – ⑧ mara mbili ama tatu.




⑦ Kunyunyizia maji




Jambo la kukumbuka
Fikiria na amua kimo kinachokufaa kuwezakupika ukiwa umesimama. Punguza kimo cha shimo la moto kufikia 30cm, na kisha unaweza kuamua kimo cha misingi na laini za matofali.

⑧ Kukandika




3. Kuunda shimo la moto


⑩ Kutengeneza pahali pa moto
(ukuta)



Mpanga wa kutengeneza
shimo la moto.





⑪ Kutengeneza shimo la kuwekea kuni.




matofari nusu ama
robo. (unakata.)

⑫ Kukandika





⑬ Kutengeneza mashimo ya kuwekea nyungu.




kupanga matofari

⑭ Kukandika na kuhakikisha kipimo cha shimo la kuni na moto.




⑮ Kutengeneza pembe za mashimo ya nyungu.




Jambo la kukumbuka
Weka sufuria au nyungu mahali panapofaa na uunde pembe za shimo ili kuwezesha shimo kufaa kwa masufuria au nyungu za ukubwa tofauti.

⑩ Kutengeneza meza ya kuni.



⑪ Kukandika na kulainisha juu kwa kutumia mwiko au kipande kidogo cha bati.




⑫ Kukausha: Funika na gunia au aina ya kitambaa ili kuwezesha kukauka polepole bila kupasuka pasika. Kunyunyizia maji kidogo kunaweza kuzuia kupasuka.

Baada ya siku 7-10 kandika kwa mavi ya ng'ombe, mchanga na maji.

Sasa umemaliza. Uanze kutumia!

Kutumia jiko la Enzaro vizuri

1. Kama inahitajika weka mawe madogo katikati ya sufuria na kando za shimo ili kuruhusu joto kupita vizuri na kuwezesha sufuria kuwa imara.
2. Wakati wa kuchemsha maji au kupika chochote kwa sufuria, ifunike ili kuzuia kupotea kwa kawi.



3. Wakati unahitaji shimo moja tu, funika njia ya joto kupitia kwa yale mashimo mengine mawili kwa kutumia matofali au mawe.



4. Ondoa majivu kwenye shimo la kupitia ulimi wa moto ili kuwezesha joto kupita vizuri.
5. Unaweza kutumia majivu kwa:-
 - Kusafisha choo.
 - Kunyunyizia kwenye shamba la mboga kama dawa ya wadudu au kama mbolea.
 - Kuzuia mchwa kwenye miche.
 - Kulainisha jiko lako ukichanganya majivu na matope.

Aina za jiko la Enzaro



Aina kamili ya Enzaro jiko lenye mashimo matatu. Shimo moja limewekwa nyungu ambayo haitolewi ili kuwezesha kupata maji yaliochemka wakati wowote.
(Bi. Peles Kabibu, Chuluni District)



Kipimo cha jiko kinafaa kwa watoto kuweza kupika.
(Bi. Peles Kabibu Chuluni Div. Tarafa ya Kitui)



Jiko lenye mashimo mbili
Matope kwenye pande ya mbele yalitolewa ili
jiko lionekane nzuri.
(Bi. Kasemba Mwambu, Chuluni Division, Tarafa ya Kitui)

Kijitabu cha kujitengenezea Jiko la Enzaro

Jiko la Enzaro limeanzishwa na Population Promotion Education Programme(PEPP)

*Kwa ushirikiano wa kikundi cha WASHA WA MUKAMBA. Wakisaidiwa na DFEO
Chuluni, Mpango wa UN-WEP-FFW walayani Kitui.*

Michoro na Bi.Yuko Takeuchi, Bw.Kuroda

Kimehaririwa na Extension method and Information section, SOFEM

Kimetolewa na Social Forestry Extension Model Development Project (SOFEM)

P.O.BOX 892, KITUI, TEL.0141-22471/22626, FAX.0141-22807